*Kioo cha Lugha, Juz. 23(2), 123-133*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam* DOI: https://dx.doi.org/10.4314/kcl.v23i2.13

## Utangulizi

# Utumwa na Maisha Baada ya Utumwa katika Jamii za Afrika Mashariki: Historia, Lugha na Fasihi ya Kiswahili

*Salvatory S. Nyanto*[1] *na Angelus Mnenuka*[2]

### 1.0 Utangulizi

Sehemu hii ya utangulizi inatoa usuli kuhusu utumwa na maisha baada ya utumwa katika jamii mbalimbali zinazopatikana katika eneo la Afrika Mashariki. Maendeleo ya hivi karibuni katika tafiti za utumwa na maisha baada ya utumwa yamechangia kuwapo kwa maandiko mbalimbali kuhusu utumwa, kukomeshwa kwa utumwa, mabadiliko kutoka katika hali ya utumwa na athari za utumwa barani Afrika katika kipindi cha karne mbili zilizopita. Kwa muda mrefu, watafiti wamekuwa wakiangazia jitihada za Waafrika za kukomesha utumwa. Hata hivyo, uchunguzi wao ulikuwa finyu kwani mawanda ya tafiti hizo yalibanwa katika mitazamo ya utaifa na usasa ambayo yanaweka kando dhana ya utumwa wenyewe na hali mbalimbali zilizojitokeza baada ya kukomeshwa kwa utumwa, kipindi kinachojulikana kitaalamu kama ubadautumwa. Kazi zilizokwishafanyika kwa miongo kadhaa hadi sasa, zimedhihirisha wazi kwamba hakukuwa na mabadiliko ya moja kwa moja kutoka hali ya utumwa hadi kupata uhuru. Watumwa waliendelea kuwa utumwani kwa miongo kadhaa baada ya utumwa kukomeshwa rasmi. Hata hivyo, kuna ruwaza zinazolandana ambazo zinaweza kupatikana katika mabadiliko hayo anuwai (Department of History, 2023). Tajiriba hizo zote za utumwa zimesawiriwa barabara katika kazi za fasihi kwa sababu fasihi ni njia mojawapo ya mawasiliano katika jamii, yaani mawasiliano ya kisanaa.

Hakika, si mawasiliano tu bali fasihi hujadili masuala yanayotendeka katika jamii kwa kuyatolea maoni, kuyakumbuka, kuyasisitiza, na wakati mwingine kukosoa. Aidha, baadhi ya mijadala inayodadisi masuala tunduizi ya utumwa na athari zake katika vipindi mbalimbali, inapatikana pia katika kazi za fasihi andishi na simulizi. Kwa mfano Lorna V. Williams na Marcus Wood wamechambua kazi za fasihi katika nchi za Brazili na Kuba (Amerika ya Kilatini) na kubainisha kuwa waandishi wa Kizungu waliligusia suala la utumwa kijuujuu

[1]Idara ya Historia, Ndaki ya Insia, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania. Baruapepe: ssnyanto@udsm.ac.tz
[2] Profesa Mshiriki, Idara ya Fasihi, Mawasiliano na Uchapishaji, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Baruapepe: amnenuka@udsm.ac.tz

ilhali waandishi weusi walijadili suala hilo kwa kina (Williams, 1994; Wood, 2019). Aidha, katika uchunguzi wake wa fasihi za utumwa nchini Uingereza, Sofia Muñoz-Valdivieso anadai kuwa fasihi zilizotungwa na vizalia vya watumwa waliotokea Karibe, zinaonesha madhila ya biashara ya utumwa na utumwa kwa kulitazama suala hili katika muktadha wa namna wahamiaji wanavyotazamwa nchini Uingereza (Muñoz-Valdivieso, 2020). Si nje ya bara la Afrika pekee, hata ndani ya bara la Afrika ambalo ni chimbuko la watumwa wengi wa Amerika, kazi za fasihi zimejadili suala la utumwa na namna linavyoibua hisia (Murphy, 2012). Ni dhahiri kuwa athari za biashara ya utumwa na utumwa bado zipo, zitaendelea kuwapo na kujadiliwa katika nyuga za historia na fasihi.

Makala katika toleo hili maalumu la jarida la *Kioo cha Lugha* zinachunguza katika mawanda mapana utumwa na athari zake katika jamii za Afrika Mashariki kwa kuweka pamoja tafiti mbalimbali za kihistoria na kifasihi zilizoandikwa kwa Kiswahili.[3] Jarida hili linatoa mwelekeo mpya kwa wanahistoria, wanafasihi, na wanataaluma wa Afrika Mashariki na ulimwenguni kwa ujumla ambao kwa muda mrefu wamekuwa wakichunguza masuala mbalimbali ya Afrika, lakini wamekuwa wakifanya hivyo kupitia mitazamo ya utaifa ambayo inaweka kando utumwa na ubadautumwa na athari zake katika jamii ya sasa ya Afrika. Aidha, makala zilizomo katika toleo hili maalumu zinaendeleza jitihada zilizokwishafanywa kuhusu utumwa katika ukanda huu wa Afrika Mashariki ambapo, licha ya kutumia lugha ya Kiafrika ya Kiswahili, makala hizi zimechambua dhana na athari ya utumwa katika mawanda mapana. Kwa kufanya hivi, mawanda ya makala hizi yanafanana na yale ya kazi za Afrika Magharibi, Amerika na Ulaya ambako tafiti nyingi kuhusu utumwa zimekwishafanyika tena kutoka katika taaluma mbalimbali.

## 2.0 Historiografia ya Utumwa, Lugha na Fasihi ya Kiswahili

Kwa zaidi ya miongo mitatu ya utoaji maarifa katika Afrika Mashariki, tafiti nyingi zimejikita katika utumwa, athari na maisha baada ya utumwa zikiegemea katika jamii za ukanda wa pwani (Morton, 1990; Glassman, 1991; McMahon, 2013). Mathalani, kazi za Abdul Sheriff zinatumia Zanzibar kama kategoria ya ulinganifu kuonesha athari za utumwa katika karne ya 19 kama "sehemu ya himaya kubwa ya kibiashara" (Sheriff, 2002: 1). Vivyo hivyo, kazi ya Frederick Cooper kuhusu utumwa katika mashamba kisiwani Zanzibar na katika pwani ya Kenya imeonesha hali za watumwa katika uchumi wa mashamba, nafasi zao katika jamii za pwani, na fursa zilizokuwapo baada ya kupitishwa kwa sheria ya kukomeshwa kwa utumwa ya mwaka 1907 (Cooper, 1997). Tafiti hizi za mwanzo zilivutia watafiti wengine kutafiti na kuandika kuhusu migomo na dini kama njia mojawapo ya kupata uhuru na utambulisho, heshima, na maisha baada ya utumwa katika jamii za pwani ya Afrika Mashariki (McMahon, 2013). Watafiti wengine, walitumia dini kama kategoria ya ulinganifu ambapo walionesha nafasi ya wamisionari wa pwani na pwani-bara, na Zanzibar katika ukomeshaji wa utumwa na uanzishaji wa vijiji vya watumwa waliokombolewa. Hata hivyo, mwitiko wa baadhi ya Waafrika ulibadilika "mara nyingi kutokana na hatua zilizochukuliwa na wamisionari kuhusu kazi katika misheni na

[3] Fasihi ni chanzo kimojawapo cha kujua historia ya jamii (taz. Klinjuy katika "A Comparative Study on theWriting Styles of Slave Narratives" ya mwaka 2011 anarejelea fasihi ya watumwa kama kazi za historia).

uinjilishaji" (Kollman, 2005: 14).

Licha ya tafiti za utumwa kuegemea zaidi katika ukanda wa pwani, kumekuwa na mabadiliko kuhusu utumwa na maeneo ya utafiti katika miaka ya hivi karibuni. Jan-Georg Deutsch na Stephen Rockel ni miongoni wa watafiti waliodhihirisha umuhimu wa tafiti katika jamii za bara, wakionesha jinsi jamii zilivyoungwa katika uchumi wa kimataifa kupitia misafara ya wapagazi, utumwa na uzalishaji mali, na ukomeshaji wa utumwa (Deutsch, 1998; Rockel, 2006). Licha ya watumwa kupata uhuru kupitia utoaji wa vyeti vya uhuru, mwisho wa utumwa ulidhihirisha ukombozi bila kukomeshwa kwa utumwa kwa sababu utumwa uliendelea na watumwa walijitahidi kufanya mazungumzo kuhusiana na kuwekwa pembezoni kijamii (Médard na Doyle, 2007). Hivi karibuni, kumekuwa na msukumo wa watafiti kuelekeza nguvu zao katika utumwa na maisha baada ya utumwa katika jamii za bara. Kazi za Salvatory Nyanto, Henri Médard and Shane Doyle ni mifano dhahiri ya mrengo huu mpya (Médard na Doyle, 2007; Nyanto, 2019). Maeneo mengine yaliyovutia watafiti yanahusu masimulizi, kumbukumbu, na tawasifu za watumwa wa kike na wa kiume, na usawiri wa utumwa katika kazi za fasihi (Henry, 2020). Kwa kujikita katika masimulizi, maisha na tawasifu za watumwa kama kategoria ya ulinganifu, tafiti kadhaa katika uga huu zimeonesha sauti za watu wa tabaka la chini, hasa watumwa ambao wamekuwa wakifichwa katika historia na masimulizi ya watumwa (Alpers, 1983; Robertson na Klein, 1989; Wright, 1993). Kuwapo kwa sauti za tabaka la watu wa chini katika kazi zinazohusu utumwa kumekuwa sehemu ya mijadala ya wanazuoni kuhusu utumwa katika jamii kwa nyakati na maeneo tofauti (Bellagamba, Greene na Klein, 2016).

Vilevile, Henry (2021) anachambua riwaya ya *Uhuru wa Watumwa* akiangazia simulizi za watumwa kupitia ruwaza, motifu na maudhui. Katika utafiti huo alichunguza jamii za Kiafrika, Kimarekani na Kizungu ambapo alibaini kwamba japokuwa miktadha ya kiutunzi ni tofauti na kumekuwapo na matumizi ya nduni tofauti kutoka jamii moja hadi nyingine, lakini simulizi za utumwa zina mambo yanayofanana na kuuona ni utanzu mahususi wa kifasihi wenye nduni anuwai za kisanaa. Tofauti na Henry, Mutembei (2001) anachambua dhamira hii ya utumwa akiangalia ni kwa namna gani watunzi wa fasihi ya Kiswahili wamelisawiri suala la utumwa kwa kipindi cha miaka hamsini. Katika kuichambua dhamira hiyo, anatumia kazi tatu ambazo ni: *Uhuru wa Watumwa* (1934), *Maisha ya Tippu Tip* (1966) na *Tendehogo* (1984).

Mjadala kuhusu sauti za watu wa kawaida katika tafiti na kazi mbalimbali umepanua wigo wa utafiti kuhusu watumwa watoro katika jamii mbalimbali za Afrika Mashariki ambao walitumia utoro kama njia ya kupata uhuru. Licha ya kuwapo kwa msukumo wa mjadala wa utoro, tafiti nyingi zimejikita katika historiografia ya utoro katika pwani ya Afrika Mashariki. Mathalani, Fred Morton anabainisha kuwa ingawa watumwa walitoroka na kuanzisha jamii za watoro, uvamizi wa kikoloni "uliongeza madhila na unyonyaji dhidi ya watoro" na kwamba "kukomeshwa kwa utumwa hakukuwa na mabadiliko ya kijamii na kiuchumi" (Morton, 1990: 2). Kwa upande wa Tanzania, tafiti kuhusu vijiji vya watumwa watoro katika maeneo ya Pangani, Saadani na Bagamoyo zinaonesha dhima ya vijiji hivyo katika uendelezaji wa fikra za uasi miongoni mwa watumwa kama nyenzo ya kupinga uonevu katika jamii; hivyo, kuanzishwa kwa jamii huru za watumwa kulidhihirisha "urazini wa uasi wa watumwa" (Glassman, 1991: 277). Hata hivyo, katika baadhi ya maeneo, tafiti zinaonesha kuwa watumwa waasi walihitaji

jamii mpya na si uhuru kwa kuwa walihitaji watu ambao wangewasaidia kujumuika na kukubalika katika jamii (Glassman, 1991). Kwa mfano, katika kitabu cha Marcia Wright, masimulizi na taarifa mbalimbali kuhusu jamii za Afrika Mashariki, Kusini na Afrika ya Kati yanaonesha kuwa kukomeshwa kwa utumwa kulichangia kuwapo kwa "kiasi cha uhuru" na kwamba mabadiliko hayo hayakuwa uhuru kamili kwani baadhi ya watumwa waliendelea kuishi kwa wamiliki ilhali wengine walipewa hifadhi katika jumuiya zilizokuwa katika misheni za Kikristo (Wright, 1993: 1).

Tafiti hizi zinadhihirisha kuwa watumwa waliendelea kuwa utumwani kwa miongo kadhaa baada ya utumwa kukomeshwa rasmi, kipindi chote cha ukombozi, na baada ya hapo. Aidha, tafiti zimedhihirisha kuwa, kuna aina nyingi za utumwa, na kwamba utumwa wa kisasa unaakisi utumwa wa kijadi katika masuala anuwai (Mulokozi, 2003; Henry, 2020). Aidha, tafiti za utumwa hazikulenga kuwasilisha maarifa kuhusu utumwa katika lugha inayotumika katika mawasiliano mapana ya jamii. Mathalani, Kiswahili ni lugha inayotumika katika mawasiliano mapana ya kijamii katika shughuli rasmi na zisizo rasmi katika eneo la Afrika Mashariki. Kwa hiyo, toleo hili maalumu ni jitihada za kuweka pamoja tafiti kutoka nyanja tofauti kama historia na fasihi zinazohusu utumwa anuwai na athari zake katika Afrika ya leo.

Kwa mintarafu ya upungufu huu katika tafiti, makala zilizowasilishwa katika toleo hili maalumu zinaziba pengo hilo kwa kuweka pamoja katika Kiswahili tafiti za hivi karibuni zinazohusu utumwa Afrika Mashariki. Makala zilizomo zinatumia mikabala mbalimbali ya utumwa, masimulizi na mifano katika jamii za Afrika Mashariki. Aidha, makala zinaangazia masuala anuwai kama vile kategoria za utumwa, hali walizopitia watumwa wakati wa utumwa na maisha yao baada ya uhuru, kukomeshwa kwa utumwa, na athari za utumwa katika jamii ya Afrika Mashariki na barani Afrika kwa ujumla katika kipindi cha karne mbili zilizopita. Kwa kuweka pamoja makala hizi katika lugha ya Kiafrika ya Kiswahili, wanafunzi, wanataaluma, na wanajamii wa Afrika Mashariki kwa ujumla watapata maarifa kuhusu utumwa na athari zake katika jamii, maarifa ambayo pengine wasingeyapata endapo makala hizi zingeandikwa kwa lugha za kigeni kama Kiingereza ambazo wengi hawazifahamu.

Toleo hili maalumu ni jitihada za kitaaluma katika kuchangia maarifa yaliyopo kuhusu utumwa kwa kuchunguza namna ambavyo fasihi kama chanzo cha kuhifadhi historia ya jamii ilivyofanikiwa kuweka wazi aina mbalimbali za utumwa zinazojitokeza katika historia ya sasa ya Afrika. Aidha, baadhi ya makala zimeweka bayana athari za utumwa katika jamii na kuonesha mapana ya dhana ya utumwa ambao bado unaendelea katika jamii na athari zake. Si hivyo tu, bali jitihada mbalimbali zinazofanyika katika kukabiliana na utumwa zimefafanuliwa. Sambamba na hayo, toleo hili maalumu linaweka pamoja tafiti hizo zinazohusu utumwa na athari zake katika Ukanda wa Afrika Mashariki kwa kutumia Kiswahili, lugha ya Kiafrika ambayo inafahamika kwa watu wengi Afrika Mashariki, hivyo, itawawezesha wanajamii wengi hata wale wasiojua lugha za kigeni kupata maarifa yanayowasilishwa kutokana na tafiti hizo. Kwa ujumla, toleo hili maalumu limezingitia umuhimu wa matumizi ya lugha za jamii za Kiafrika katika kuwasilisha masuala mbalimbali yale yanayohusu jamii husika, hususani suala nyeti kama utumwa lililoacha athari kubwa za kijamii, kiuchumi na kisiasa katika jamii nyingi za Kiafrika.

Ili kukamilisha yote haya, tafiti za hivi karibuni kuhusu utumwa kutoka nyanja

mbalimbali za kitaaluma kama vile historia na fasihi ziliwasilishwa kwa lugha ya Kiswahili katika Kongamano la Utumwa na Maisha baada ya Utumwa katika Historia ya Kisasa ya Afrika lililofanyika katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mwaka 2023, na zile ambazo hazikuwasilishwa katika kongamano hilo, zimewekwa pamoja katika jarida hili. Michango mbalimbali kutoka kwa wanataaluma na wanazuoni wa masuala ya utumwa imekuwa na umuhimu mkubwa katika kuongeza maarifa na kuboresha tafiti zilizowasilishwa. Kwa ujumla, kumekuwa na uhaba mkubwa wa machapisho ya kitaaluma katika lugha ya Kiswahili hata kwa watafiti wanaotumia lugha ya Kiswahili katika mawasiliano yao ya kila siku. Suala hili linawakosesha watumiaji wa lugha ya Kiswahili kupata maarifa mbalimbali kama wanayoyapata wazungumzaji wa Kiingereza kwa mfano. Hakika, suala hili ni aina nyingine ya utumwa wa lugha unaojadiliwa na Aldin Mutembei katika toleo hili maalumu. Ndiyo maana toleo hili maalumu limeandaliwa ili kukidhi haja hiyo kubwa ya kuchapisha tafiti kuhusu utumwa katika andiko moja kwa lugha ya Kiswahili ili kuwaletea maarifa watumiaji wa lugha ya Kiswahili wanaopenda kufuatilia masuala ya utumwa barani Afrika. Aidha, makala hizi zitawarahisishia wanazuoni, wanataaluma, na wanafunzi kupata uelewa mpana wa dhana ya utumwa pamoja na kupanua fikra zao kuhusu hali ya utumwa barani Afrika katika kipindi cha karne mbili zilizopita mpaka sasa.

**3.0 Muhtasari wa Makala: Historia, Fasihi na Lugha ndani ya Jarida Hili**

Utumwa umekuwapo katika jamii kwa muda mrefu kama mfumo wa kijamii wa kumiliki watu na kutumwa bila malipo yoyote (KKS, 2014). Ni hali ya kumiliki watu na kuwafanyisha kazi bila kuwapa ujira. Makala ya Elizabeth Mahenge ikiongozwa na Nadharia ya Naratolojia imechambua tamthiliya ya Edwin Semzaba ya *TENDEHOGO* inayoelezea jinsi biashara ya watumwa ilivyofanywa na wafanyabiashara Waarabu na wenyeji katika Afrika Mashariki wakati wa karne ya 18 na 19. Tamthiliya inasimulia kuhusu uzoefu wa watumwa wa Kiafrika wakinyanyaswa na kupelekwa Bara Hindi ambako ni mbali na kwao. Mwandishi anatumia 'sauti za usimulizi' kama mbinu ya kuibusha dhamira katika kazi za kifasihi. Kwa kutumia Nadharia ya Naratolojia, mwandishi anadhihirisha mtazamo wa msimulizi anayesimulia hadithi yake na hivyo kuwawezesha wasomaji kufahamu ni nani anayeongea kama ni msimulizi-mhusika, msimulizi aliye nje ya usimulizi, au wakala anayeachwa na msimulizi. Pamoja na mambo mengine, nadharia hii imemuwezesha mwandishi kuhakiki namna jinsia inavyoathiriwa na kazi za mtunzi kwani, mwandishi anaamini, jinsi za waandishi huathiri matini wanazozitunga.

Mjadala kuhusu maana ya utumwa umekuwa ukienda sambamba na mitindo mbalimbali ya utumwa. Kuwapo kwa biashara ya watumwa kati ya Afrika Mashariki na Afrika ya Kati kulichangia kuingia na kukua kwa Kiswahili katika mikoa ya Mashariki mwa Kongo (kama inavyofahamika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo). Hadi leo, wakazi wa mikoa ya Mashariki ya Kongo hutumia lugha ya Kiswahili pamoja na lugha nyingine za Kibantu kama lugha za mawasiliano. Makala ya Kalunga Mwela-UBI Marcel na Kilongozi Si Umba Jean inatuonesha kuwa hapo zamani mataifa au jamaa zilizokuwa na nguvu ziliweza, kwa malengo tofauti, kuzifanya baadhi ya jamii au makundi fulani ya watu kuwa watumwa. Kwa kutumia lugha ya Kiswahili kama kategoria ya uchambuzi,

waandishi hawa wanabainisha biashara ya watumwa iliyofanyika hapo kale ikitokea, au vyema zaidi, ikipitia Afrika Mashariki na kuzilenga jamii au watu weusi wa maeneo kadhaa ya nchi ya Kongo. Tofauti na makala nyingine katika jarida hili, makala hii inachunguza biashara ya utumwa kama njia mojawapo iliyochangia kuingia kwa lugha ya Kiswahili nchini Kongo. Lengo la makala hii ni kuonesha kwamba katika maeneo ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo yaliyokumbwa na biashara hii, maneno mengi ya Kiswahili yalipata kuathirika kutokana na mazingira mapya yalimokaribishwa. Waandishi wanatumia isimu linganishi kati ya Kiswahili cha Afrika Mashariki na kile cha Kongo kuchunguza kwa kina kuenea kwa Kiswahili katika karne ya 19 na 20 kwa kuangazia zaidi *Fonolojia*, *Mofolojia, Leksikolojia* na *Semantiki*.

Ni wazi kwamba utumwa umeendelea kuwapo katika jamii ukijidhihirisha katika sura na muktadha tofauti. Licha ya kuwapo kwa aina mbalimbali za utumwa, Ernesta Mosha na Grace Minja wanakiri kuwa kuna aina kuu mbili za utumwa: utumwa wa kimapokeo na utumwa wa kisasa. Utumwa wa kimapokeo unahusu watu kuuzwa kama bidhaa na kwenda kutumikishwa sehemu kama vile kwenye mashamba makubwa, migodini na nyumbani, na umekuwapo katika jamii kwa muda mrefu. Madhara ya utumwa wa kimapokeo bado hayajafutika katika historia za jamii husika. Kwa upande mwingine, utumwa wa kisasa ni utumwa unaojitokeza kwa namna nyingi kama vile: utumwa wa kifikra, kimapenzi, kiuchumi kutumikisha watoto wadogo, utumwa wa kidini na utumwa wa madeni. Kwa mantiki hiyo, waandishi wanatumia Nadharia ya Mwingilianomatini, riwaya nne za fasihi ya Kiswahili ambazo ni *Uhuru wa Watumwa* (1934), *Kasri ya Mwinyi Fuad* (1987), *Kwaheri Iselamagazi* (1992) na *Miradi Bubu ya Wazalendo* (1995) kuchunguza kategoria za utumwa katika jamii za Afrika Mashariki. Matumizi ya Nadharia ya Mwingilianomatini inawasaidia waandishi kuonesha kwa kina namna fasihi ya Kiswahili inavyosawiri utumwa wa kijadi na aina anuwai za utumwa wa kisasa. Vilevile, nadharia imesaidia kubaini kuwa madhara ya utumwa wa kisasa ni makubwa kuliko yale ya utumwa wa kimapokeo kwa sababu hayaonekani waziwazi kwa kuwa yapo ndani ya utu wa mhusika. Aidha, waandishi wamebaini kuwa utumwa wa kisasa, hususani utumwa wa kifikra na utumwa wa madeni unachangia kuimarishwa kwa utumwa wa kijadi katika jamii.

Ingawa simulizi ya *Uhuru wa Watumwa* imevutia tafiti kadhaa, kuna simulizi kadhaa zilizoandikwa na wanawake. Makala ya Tom Olali, ambayo imejikita katika kisiwa cha Pate kilichoko kaunti ya Lamu, inakoleza mada kuhusu masuala ya kijinsia kwa kuchambua *Utendi wa Mwanakupona*. Utenzi huu mashuhuri ulitungwa na mwanamke, Mwanakupona binti Mshamu Nabhany akimnasihi na kumshauri binti yake Mwana Hashima bint Shee Mataka jinsi ya kuwa mke mwema kwa mumewe. Ingawa, tafiti kadhaa zimeuchambua utenzi huu kwa kuangalia masuala mbalimbali kama vile utumwa wa kimawazo au utumwa wa ukandamizaji wa wanawake, makala ya Olali yanaiangalia motifu ya utumwa na utabaka katika kisiwa cha Pate, Lamu, kwa muktadha wa watumwa kama ilivyokuwa katika biashara ya watumwa. *Utendi wa Mwanakupona* unamsaidia mwandishi kuchanganua umuhimu wa kuelewa utumwa si tu kama sehemu ya historia ya jamii za pwani ya Afrika Mashariki bali pia kama masimulizi yenye nguvu ambayo yanaendelea kuvuma katika matini za fasihi ya Kiswahili. Vilevile, utendi huu umesawiri ufahamu wa kina wa athari za utumwa, ukiangazia jukumu lake katika kujenga

utambulisho wa kitamaduni na kukuza diskozi za kijamii katika mapambano yanayoendelea ya haki, utambuzi na utambulisho katika jamii kwa makundi, watu na wajoli wa watumwa.

Njia mojawapo ya kusafirisha watumwa kutoka barani Afrika ilikuwa usafiri wa maji. Watumwa kutoka Afrika walisafirishwa kupitia Bahari ya Hindi kwa upande wa upwa wa Afrika Mashariki, na Bahari ya Atlantiki kwa upande wa Afrika Magharibi. Wakiwa safarini, kutokana na sababu kadha wa kadha, watumwa walikumbana na matendo na masuala mbalimbali ambayo yamesawiriwa kwa taswira mbalimbali katika kazi za fasihi. Shani Mchepange na Grace Minja wanajadili taswira mbalimbali za bahari kama zinavyosawiriwa katika riwaya ya *Uhuru wa Watumwa* (1934) iliyoandikwa na James Mbotela. Wakiongozwa na Nadharia ya Udenguzi ya Jacques Derrida, katika uchambuzi wa riwaya husika, waandishi wamebainisha taswira zilizosawiriwa katika makundi mawili: kundi lenye jozi kinzani ambalo lina taswira za usalama na hatari au kifo, uhuru na utumwa, na muungano na utengano. Kundi lingine lina taswira zingine zinazoonesha athari za biashara ya watumwa, mchango wa watumwa katika maendeleo ya uchumi duniani, kuibua hisia kwa msomaji, na kusawiri mandhari ya biashara ya watumwa.

Ingawa tatizo la utumwa hufikiriwa kuwa ni la zamani, utumwa bado upo na unadhihirika kwa sura mbalimbali. Makala ya Lina Akaka inatumia tamthiliya ya *Jeneza Kutoka Saurabia* iliyoandikwa na Wa Mberia (2025) ili kuchunguza namna mwanamke anavyotumikishwa. Makala inaongozwa na mkabala wa Bales (1999) wa haki za binadamu na utandawazi kwa kuchunguza tajiriba za mwanamke katika utumwa pamoja na madhila yake ndani ya karne ya 21, hususani katika mataifa ya Mashariki ya Kati. Uchunguzi wa tamthiliya hii pamoja na mambo mengine, unaonesha kuwa utumwa bado unaendelea na wanawake, kwa kiasi kikubwa, wamekuwa wahanga wa mfumo huu dhalimu. Kwa kutumia Nadharia ya Uhalisia, mwandishi anaonesha tajiriba za mwanamke wa Kiafrika katika utumwa na umuhimu wa watafiti na watetezi wa haki za binadamu kuchunguza aina nyinginezo za utumwa zinazojitokeza katika kazi za fasihi. Pamoja na mambo mengine, makala ya Akaka inaonesha kuwa ingawa hatua kubwa zimepigwa katika diskosi za haki za wanawake ulimwenguni, aina tofauti za utumwa wa wanawake zimekuwa bayana katika karne ya 21 zikihusisha ukandamizaji, ubidhaishaji wa wanawake ambao umefichika katika taasisi za sasa, kaida za kitamaduni, na mifumo nguvu ya kibabedume.

Kwa ujumla, kumekuwa na masimulizi tofauti kuhusu madhila ya utumwa katika Afrika Mashariki—bila kujumuisha visiwa vya Zanzibar. Watumwa pamoja na vizazi vyao walisimilishwa katika jamii ilhali wengine wakijiunga na Ukristo na Uislamu kama mojawapo ya jitihada zao za kupoteza utambulisho wao wa utumwa. Baadhi walijishughulisha na shughuli za uzalishaji mali, wengine wakiyahama makazi na kuanzisha miji na vijiji vya mbali ili kuficha aibu ya utumwa. Hata hivyo, licha ya kuwapo kwa fursa anuwai kwa watumwa na vizazi vyao, bado imekuwa changamoto kuzungumzia kuhusu historia ya utumwa. Makala ya Salvatory Nyanto inaongozwa na Nadharia za Naratolojia na Udenguzi kujadili kuhusu simulizi za utumwa na aibu katika jamii za Unyamwezi. Mwandishi anaonesha kuwa wajoli wa watumwa pamoja na wazee katika vijiji na miji ya Tabora waliohojiwa hawakuwa tayari kuzungumza kuhusu utumwa. Wengine hawakuwa tayari kuhojiwa ama kushiriki katika mazungumzo kuhusu utumwa kwani ni aibu kuuzungumzia utumwa ambao kwa mujibu wa utumaduni wa Wanyamwezi

ni mwiko. Baadhi ya wajoli wa utumwa walitaradadi kusimulia utumwa ili kukwepa aibu na kulinda heshima na ushawishi wao katika jamii. Wengine walibadili majina yao kama njia ya kuficha utambulisho na asili zao. Aidha, matokeo ya utafiti yanadhihirisha kuwa utumwa umeendelea kuwa jambo la aibu na fedheha katika jamii za Wanyamwezi na unaathiri mahusiano ya watu katika jamii. Katika makala hii, mwandishi anatumia aibu kueleza kwa kina ugumu wa kufanya utafiti kuhusu utumwa katika karne ya 21. Kwa kutumia simulizi za watumwa wa kike wawili, makala hii inaeleza changamoto za kusimulia masuala ya utumwa katika jamii ambayo ilikuwa vigumu kuwasilimisha watumwa ili wawe na hadhi kama wengine.

Utumwa-lugha ni miongoni mwa athari za utumwa ambazo zimeendelea kuwapo katika jamii. Makala ya Aldin Mutembei inaongozwa na mawazo ya Frantz Fanon kuhusu lugha (2008), akitumia dhana ya *utumwa-lugha* kujadili jinsi lugha za watawala wa kikoloni barani Afrika zinavyotokeza utumwa wa kifikra, ambao hatimaye unaharibu misingi mikuu ya kuwako kwa Mwafrika. Kupitia *utumwa-lugha*, Mutembei anaonesha kuwa Waafrika wameachwa katika mtanziko mkubwa wenye mivutano ya ndani inayojibadilisha kuwa minyiri isiyoweza kukatwa na kung'olewa bila ya kuwa na mapinduzi ya kifikra. Kwa mujibu wa Mutembei, ingawa maana ya utumwa imekuwa katika mijadala ya wanazuoni hasa baada ya mwaka 1926 hadi mwaka 2012, bado kulikuwa na mjadala wa kisheria kuhusu maana ya utumwa. Mijadala hii haikuangalia sana suala la lugha kama lenye kuingiza dhana ya kipekee katika maana ya utumwa. Hata hivyo, ni wazi kuwa wakati wa utumwa wa Waarabu, lugha ilitumika kuufanikisha utumwa—kwa kuubeba utumwa. Wakati wa ukoloni mkongwe, lugha za kikoloni zilijenga matabaka ya kitumwa. Minyiri ya utumwa-lugha ikajiviringa na kuwavunganiza watumwa kifikra na kuwafanya wajikane. Wakati huu wa ukoloni mamboleo, utumwa-lugha umeifanya fikra ya aliyetawaliwa kushikwa na minyiri ya kikoloni kiasi cha kujikuta katika mtanziko: alikotoka hakujui na, kama kuna aendako, hakufahamu. Kwa waliotawaliwa na Waingereza, (ni sawa kwa waliotawaliwa na Wafaransa, Wareno au Wahispania) asipofahamu Kiingereza, huyo ni mjinga, mbumbumbu, hana akili. Lakini akija mtu ambaye Mwingereza hakumtawala, na huyo mtu pia hajui Kiingereza, anaangaliwa kwa heshima na staha na wale waliotawaliwa. Kiingereza kimewaweka Waafrika katika mtanziko wa kifikra.

Hoja kuhusu athari za utumwa na ukoloni inaendelezwa katika makala ya Hamisi Chembea ambayo inajikita katika fasihi ya Kiswahili kwa kuchunguza manyezi ya utumwa katika makutano ya utumwa na ukoloni na athari zake kwa usemi wa kitamaduni na mitazamo ya jamii. Mwandishi anaonesha kuwa fasihi ya Kiswahili imekuwa chemchemi ya kueleza sauti za waliotengwa, kutambua hali halisi ya maisha ya utumwa, upinzani na ustahimilivu. Uchunguzi huu pia umeshughulikia makutano ya ukoloni na utumwa, ukionesha jinsi nguvu hizi zinavyoingiliana ili kuathiri usemi wa kitamaduni na mitazamo ya jamii. Mwandishi anatumia diwani ya Abdilatif Abdalla, *Sauti ya Dhiki* na riwaya ya Adam Shafi, *Kasri la Mwinyi Fuad,* ndani ya mifumo mipana ya kihistoria, kuonesha mateso ya kihisia-moyo na ya kimwili ya watumwa, hasa katika kuangazia mapambano yao ya kupata uhuru na utu. Chembea anachunguza umuhimu wa kuelewa utumwa si tu kama ukweli wa kihistoria bali kama masimulizi yenye nguvu ambayo yanaendelea kuvuma ndani ya kadhia za fasihi ya Kiswahili. Hatimaye, uchunguzi huu wa Chembea

unasawiri ufahamu wa kina wa athari za utumwa, ukiangazia jukumu lake katika kujenga utambulisho wa kitamaduni na kukuza diskozi za kijamii katika mapambano yanayoendelea ya haki na utambuzi.

Makala ya Angelus Mnenuka inaendeleza mjadala kuhusu athari za utumwa. Kwa kutumia uchunguzi wa kifani katika riwaya ya *Miradi Bubu ya Wazalendo* ya Gabriel Ruhumbika, mwandishi anabainisha sura za utumwa zilizofubazwa kimsamiati, hususani katika manamba. Mwandishi anatumia manamba kama kategoria ya uchanganuzi kuonesha kuwa Afrika iliathiriwa vibaya kutokana na maendeleo ya ubeberu barani Ulaya, utumwa na ukoloni vikiwa ni miongoni mwa athari hizo. Matukio haya yaliathiri Afrika kiuchumi na kumwondolea mtu mweusi hadhi ya ubinadamu. Kwa upande wa Afrika Mashariki, inadaiwa kuwa Waingereza walitokomeza biashara ya utumwa. Pamoja na sababu kuntu za kiuchumi, inaelezwa kuwa biashara hiyo ya binadamu ilipingwa kwa sababu za kiutu. Dai hili linadokeza huruma ya Waingereza kwa watumwa wa Kiafrika. Hata hivyo, mfumo wa manamba, unaelekea kuwa na sifa za utumwa kutokana na namna manamba walivyotendwa na kutendewa. Ili kuonesha bayana namna utumwa ulivyodhihirika katika manamba, Mnenuka anajadili kwa kina vipengele vya utumwa kama vinavyosawiriwa katika riwaya ya *Miradi Bubu ya Wazalendo*.

Makala ya Leonard Bakize inabainisha kuwa ingawa wachambuzi wa fasihi ya Kiswahili wamekuwa wakichambua masuala mbalimbali ya kijamii yanayowahusu watoto kwa kuchambua kazi mahususi za watoto, historia ya utumwa na ujio wa wakoloni nchini Tanzania imewavutia wanahistoria kuijadili kwa malengo tofauti. Tofauti na makala nyingine katika jarida hili, makala ya Bakize inachunguza ushiriki wa watoto katika vita dhidi ya utumwa na ujio wa wakoloni nchini Tanzania kupitia uchambuzi wa kazi teule za fasihi ya watoto na mwitiko wa wasomaji wa matini hizo. Tofauti na mtazamo wa kijamii unaowaona watoto kama kundi lisilo na sauti katika masuala mazito ya kihistoria, makala hii inathibitisha kwamba watoto walihusika moja kwa moja katika matukio hayo, ama kama wahanga, washiriki, au wahifadhi wa kumbukumbu za kijamii. Licha ya kuwapo kwa mtazamo wa kijamii unaowaona watoto kama kundi lisilo na sauti katika masuala mazito ya kihistoria, makala hii inathibitisha kwamba watoto walihusika moja kwa moja katika matukio hayo, ama kama wahanga, washiriki, au wahifadhi wa kumbukumbu za kijamii. Mwandishi amefanya utafiti kwa kupitia usomaji makini wa matini na majadiliano ya vikundi vya watoto wa shule za msingi pamoja na uchambuzi wa kazi teule hususani *Wimbo wa Sokomoko* (1990) ya Amandina Lihamba pamoja na riwaya tatu za Mugyabuso Mlinzi Mulokozi, ambazo ni *Ngoma ya Mianzi* (1991), *Ngome ya Mianzi* (1991) na *Moto wa Mianzi* (1996). Mwandishi ameongozwa na Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji na Nadharia ya Jumuiya Zilizobuniwa kuchunguza ushiriki wa watoto katika vita dhidi ya utumwa, ujio wa ukoloni na ujenzi wa taifa. Nadharia hizi mbili zinaonesha kuwa sauti za watoto zina mchango muhimu katika ujenzi wa kumbukumbu na uelewa wa pamoja wa jamii, hivyo, hazina budi kupewa nafasi stahiki katika tafiti za kifasihi na kihistoria kuhusu Tanzania na Afrika kwa ujumla.

Makala ya Jaquiline Moshi na Titus Ombori inachunguza makovu ya kisaikolojia ya utumwa kwa jamii za Kitanzania kwa kutumia masimulizi ya kihistoria, simulizi za kifamilia na urithi wa kitamaduni kama vyanzo vya msingi vya uelewa wa pamoja wa kihistoria. Kwa kutumia mbinu ya uchambuzi wa kimada, waandishi wanachambua data

kutoka katika maandiko ya kihistoria, nyaraka za makavazi na simulizi za watu binafsi kuhusu utumwa ili kubaini fadhaa ya kihistoria, urithishaji wa maumivu ya kihisia, udhalilishaji wa utu na ustahimilivu wa kijamii. Waandishi wanatumia Nadharia ya Utambulisho wa kijamii na Nadharia ya Kumbukumbu ya Kihistoria kufafanua jinsi historia ya utumwa inavyoathiri utambulisho wa mtu binafsi na wa pamoja, pamoja na ustawi wa kisaikolojia wa vizalia. Vilevile, waandishi wanatumia Nadharia ya Fadhaa ya Kizazi (*intergenerational trauma*) kueleza namna maumivu ya kihistoria yanavyorithishwa kupitia masimulizi ya kifamilia, mila na uzoefu wa kijamii. Matokeo ya makala hii yanaonesha kuwa athari za kisaikolojia za utumwa bado zinaendelea kudhihirika katika jamii za Kitanzania kupitia msongo wa mawazo, huzuni ya muda mrefu, hisia za kutengwa kijamii na mkanganyiko wa utambulisho.

## Marejeleo


Abdalla, A. (1973). *Sauti ya Dhiki*. Nairobi: Oxford University Press.

Alpers, E.A. (1983). "The Story of Swema: Female Vulnerability in Nineteenth-Century East Africa". Katika C. Robertson na M. Klein (Wah.), *Women and Slavery in Africa*. Madison: The University of Wisconsin Press.

Bales, K. (1999). *Disposable People: New Slavery in the Global Economy*. Berkley: University of California Press.

Bellagamba, Green, A.S.E. na Martin, A.K. (Wah.) (2016). *African Voices on Slavery and Slave Trade, Volume 2: Essays on Sources and Methods.* Cambridge: Cambridge University Press.

Cooper, F. (1997). *Plantation Slavery on the East Coast of Africa.* Portsmouth, NH: Heinemann.

Department of History (2023). "Call for Papers: Slavery and Post-Slavery in Modern African History". University of Dar es Salaam. Tarehe 31 Machi 2023.

Deutsch, J. (1998). "The 'Freeing' of Slaves in German East Africa: The Statistical Record, 1890-1914". *Slavery and Abolition: A Journal of Slave and Post-Slave Studies*, 19(2): 109-132.

Fanon, F. (2008). *Black Skin, White Masks*. Toleo jipya.. London: Pluto Press.

Glassman, J. (1991). "The Bondsman's New Clothes: The Contradictory Consciousness of Slave Resistance on the Swahili Coast". *Journal of African History*, Juz. 32(2), 277-312.

Glassman, J. na Glassman, J.P. (1995). *Feasts and Riot: Revelry, Rebellion, and Popular Consciousness on the Swahili Coast, 1856-1888.* Portsmouth, NH: Heinemann.

Guha, R. na Spivak, G.C. (Wah.) (1988). *Selected Subaltern Studies.* New York: Oxford University Press.

Henry, G. (2020). "Uchambuzi Linganishi wa Ujumi wa Kifasihi katika Simulizi Teule za Watumwa kutoka Afrika, Amerika na Ulaya". Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Kollman, P.V. (2005). *Evangelization of Slaves and Catholic Origins in Eastern Africa.* Maryknoll, NY: Orbis Books.

Lihamba, A. (1990). *Wimbo wa Sokomoko.* Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

McMahon, E. (2013). *Slavery and Emancipation in Islamic East Africa: From Honor to Respectability.* Cambridge: Cambridge University Press.

Nyanto, S. S. (2024). *Slave Emancipation, Christian Communities and Dissent in Post-Abolition Tanzania, 1878-1978,* London: James Currey.

Rockel, S.J. (2006). *Carriers of Culture: Labor on the Road in Nineteenth-Century East Africa.* Portsmouth, NH: Heinemann.

Shafi, A. (1978). *Kasri ya Mwinyi Fuad*. Nairobi: Vide–Muwa Publishers Limited.

Sheriff, A. (2002). *Slaves, Spices and Ivory in Zanzibar: Integration of an East African Commercial Empire into the World Economy, 1770-1873.* Oxford: James Currey.

Médard, H. na Shane, D. (Wah.) (2007). *Slavery in the Great Lakes Region of East Africa.* Athens: Ohio University Press.

Morton, F. (1990). *Children of Ham: Freed Slaves and Fugitive Slaves on the Kenya Coast, 1873- 1907.* Boulder, San Francisco: Westview Press.

Mulokozi, M. (1991). *Ngoma ya Mianzi*. Morogoro: ECOL Publications.

Mulokozi, M. M. (1991). *Ngome ya Mianzi.* Dar es Salaam: MPB Enterprises.

Mulokozi, M. M. (1996). *Moto wa Mianzi.* Morogoro: Ecol Publishers.

Muñoz-Valdivieso, S. (2020). "Slavery Fiction in Britain." *Journal of European Studies.* 50(2): 193-209. https://doi.org/10.1177/0047244120918481.

Murphy, L. (2012). *Metaphor and the Slave Trade in West African Literature*. Western African Studies. Athens, Ohio: Ohio University Press.

Wright, M. (1993). *Strategies of Slaves and Women: Life-Stories from East/Central Africa.* London: James Currey.

Mirza, S. na Strobel, M. (Wah. na Waf.) (1989). *Three Swahili Women: Life Histories from Mombasa, Kenya*. Bloomington: Indiana University Press.

Williams, L.V. (1994). *The Representation of Slavery in Cuban Fiction*. Columbia: University of Missouri Press.

Wood, M. (2019). *The Black Butterfly: Brazilian Slavery and the Literary Imagination*. Morgantown: West Virginia University Press.